

# Buriani Nabhany

Buriani natamka, kwa insali wa Manani,  
Tama zetu tunashika, kuonyesha ya huzuni,  
Mzee katuondoka, shekhe wetu Nabhany,  
Lala pema pa peponi, tupo njia twakufata.

Bara zima tunalia, hata inchi za ulaya,  
Shaha kutuondokea, na ukiwa kutwachiya,  
Wole Soyinka alia, pia Sengo analiya,  
Lala pema pa peponi, tupo njia twakufata.

Duniani tu safari, sisi sote tu wageni,  
Masikini matajiri, wenye hadhi pia duni,  
Profesa kalidhihiri, shehe Babu Nabhany,  
Lala pema pa peponi, tupo njia twakufata.

Ulikuwa mualimu, ulosheni ya ilimu,  
Liwafunza mahirimu, wanafunzi kwa walimu,  
Wema wako utadumu, japo chema hakidumu,  
Lala pema pa peponi, tupo njia twakufata.  
Ramadhan Abdallah Savonge,

*"Malenga Wa Nchi Kavuu",  
Chuo Kikuu SEKU, Kitui*